JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Posta,
S.L.P. 2599,
33101 MWANZA,
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.
www.pccb.go.tz

MWANZA – DISEMBA , 2022

UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO WAONGEZA UBORA KATIKA MIRADI YENYE THAMANI YA BILIONI 16.2

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Julai hadi Septemba, 2022 ambapo mkazo uliwekwa katika kufatilia matumizi ya fedha za Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi ya Vijiji, Mitaa, Kata na Wilaya ndani ya Mkoa. Utekekelezaji wa majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

1.1 UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi cha Julai-Septemba, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza kupitia dawati la UZUIAJI RUSHWA, imefuatilia utekelezaji wa miradi ishirini na saba **(27)** yenye thamani ya **Sh. Bil 16.2 (16,150,229,986/=)**

MCHANGANUO WA MIRADI KISEKTA NA THAMANI YAKE

Na	**KITUO**	**JUMLA YA MIRADI**	**MCHANGANUO YA MIRADI ILIYOTEMBELEWA KISEKTA**			
			SEKTA YA AFYA	SEKTA YA ELIMU	SEKTA YA UJENZI	SEKTA YA MAJI
1	MWANZA MKOANI	14	11	03	-	-
2	ILEMELA	02	01	-	01	-
3	MAGU	03	-	03	-	-
4	UKEREWE	02	02	-	-	-

5	SENGEREMA	02	01	01	-	-
6	MISUNGWI	02	-	01	01	-
7	KWIMBA	02	01	-	-	01
JUMLA KUU		**27**	**16**	**08**	**02**	**01**
THAMANI YA FEDHA		16,150,229,986	5,020,216,724	5,757,799,452	734,306,960	4,637,906,850

Aidha, **miradi yote 27** inaendelea na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na kwa baadhi ya miradi iliyoonekana kuwa na dosari hasa;

- Ucheleweshwaji wa vifaa tiba kwenye miradi 10 katika Taasisi ya Tiba Bugando inayotekelezwa chini ya mpango wa UVIKO 19 na ilishauriwa kuhakikisha vifaa vinafika na kufungwa kwa wakati ili kazi iendelee kama ilivyopangwa na tayari utekelezaji umeshafanyika.
- Aidha miradi 3 ya ujenzi wa matundu ya vyoo, ujenzi wa Bweni katika shule ya Sekondari Nyamagana pamoja na jengo la OPD Hospitali ya Fumagila Nyamagana inayofadhiliwa na TASAF kulikuwepo na changamoto ya kufungwa kwa mfumo wa malipo ambapo ushauri umetolewa na changamoto hiyo imetatuliwa na miradi inaendelea.

1.2 UCHAMBUZI WA MIFUMO

Moja ya kazi za TAKUKURU kupitia jukumu lake la Kuzuia Rushwa nchini ni kufanya udhibiti wa mianya ya rushwa kwenye Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali kwa kuchambua mifumo ya utendaji kazi kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa ili kutoa ushauri wa namna bora ya kutoa huduma na kuepuka vitendo vya rushwa.

Katika kipindi cha Julai-Septemba, 2022 Jumla ya **Chambuzi za Mifumo Sita (06)** zimefanyika katika sekta ya mapato, maji, usafirishaji, madini, ujenzi na biashara.

Kwenye chambuzi hizo, eneo mahususi TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imefanya udhibiti na kuziba mianya ya rushwa kwenye ukusanyaji wa ushuru wa madini ujenzi (mchanga, kokoto, mawe na moram) ambapo jitihada hizo zimezaa matunda na Halmashauri husika kukusanya mapato kiasi cha **Sh. 477,137,107.06/=** katika kipindi cha Julai-Septemba, 2022.

Uchambuzi wa mfumo kuhusu mianya ya rushwa kwenye ukusanyaji mapato ya madini ujenzi

Na	CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA	MAFANIKIO/HATUA YA UTEKELEZAJI
1	Halmashauri kutokuwa na mapato yaliyokusanywa kutokana na ushuru wa madini ujenzi kwenye maeneo ya machimbo na kwenye vizuizi.	Katika kipindi cha Julai-Septemba 2022, kwa Halmashauri ya Misungwi, Kwimba na Sengerema tayari wamekusanya Jumla ya **Sh. 477,137,107.06/=** mapato ambayo awali hayakuwahi kukusanywa kutokana na ushuru wa madini ya ujenzi.
2	Kutokuwepo kwa maeneo maalum ya uchimbaji wa madini ya ujenzi na kusababisha uwepo wa machimbo holela usiofuata utaratibu	Udhibiti huo umesaidia baadhi ya Halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya uchimbaji wa madini ujenzi ili kuepuka uchimbaji holela.
3	Wafanyabiashara wengi wa madini ujenzi kutokuwa na leseni wala vibali vya uchimbaji	Vibali na Leseni kwa ajili ya uchimbaji madini ya ujenzi sasa vinatolewa kwa mujibu wa utaratibu
4	Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi ya idadi za vifusi vya mchanga, mawe na kokoto zinazotolewa kwenye maeneo ya machimbo kwa siku.	Taratibu za kuwepo na kumbukumbu katika ukusanyaji ushuru na udhibiti wa mapato zimewekwa kwenye baadhi ya maeneo ya machimbo na vizuizi.
5	Wakandarasi kutolipa ushuru wa madini ujenzi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.	Baadhi ya wakandarasi wameshaanza kulipa kwa mujibu wa utaratibu.

Aidha, zipo changamoto zilizobainika kwa kila chambuzi, hivyo vikao vya warsha (**06**) vimefanyika kwa lengo la kujadili na wahusika na kuwekeana maazimio na makubaliano ya pamoja kwa ajili ya utekelezaji kwa yote yaliyobainika ili kuboresha mifumo na utoaji wa huduma.

2.0 ELIMU KWA UMMA

Elimu imetolewa kwa kuyafikia makundi mbalimbali, ambapo Semina 39 zimefanyika, mikutano ya hadhara 21, maonesho 10, vipindi 4 vya redio vimerushwa na Uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa 30 katika shule za Msingi na Sekondari na Vyuo kama ilivyoainishwa hapa chini:

Na	KAZI	UFAFANUZI
1	Elimu kwa njia ya Semina imetolewa kwa watumishi wa Serikali na sekta binafsi	Elimu imetolewa kwa watumishi kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi bila kuwepo kwa vikwazo vya rushwa pamoja na umuhimu wa kuzingatia maadili na kudumisha uzalendo kwa watumishi ili kuepuka vitendo vya rushwa. Semina hizi zimetolewa katika sekta ya Afya, Mawasiliano, Elimu, NIDA, Biashara na Ujenzi
2	Kuimarisha klabu za wapinga rushwa na vikundi vya SKAUTI katika shule za msingi, sekondari na vyuo	Uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa ni kazi endelevu inayofanywa na TAKUKURU Mkoa wa Mwanza yenye lengo la kuwakuza vijana katika misingi ya uadilifu, kuwajengea uzalendo ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye mapambano dhidi ya rushwa.
3	Kufanya mikutano ya hadhara kwa wananchi	Elimu ya madhara ya rushwa kwenye sensa ya watu na makazi imetolewa kwa wananchi ili waweze kushiriki katika kuhesabiwa pasipo kushawishiwa kwa kupewa rushwa na kurubuniwa kutokushiriki zoezi hilo. Makundi yaliyoelimishwa ni wakulima,wafugaji,wafanyabiashara, wanafunzi na watumishi wa idara mbalimbali
4	Kushiriki mbio za mwenge wa Uhuru Julai, 2022	TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imeshiriki kwenye mwenge wa Uhuru na kufikisha elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi kwa kuzishirikisha klabu za wapinga rushwa kufikisha ujumbe wa kukemea vitendo vya rushwa kwa njia ya nyimbo, ngonjera ,mashairi pamoja na kufanya maonesho na kugawa machapisho mbalimbali yenye kukemea vitendo vya rushwa.
5	Kushiriki kwenye	Kushiriki maonesho ni njia inayotumiwa na TAKUKURU

	maonesho ya wafanyabiashara Afrika mashariki na maonesho ya wakulima nanenane.	ili kufikisha ujumbe wa makatazo dhidi ya rushwa kwa wananchi. Kupitia maonesho haya wananchi wameelimishwa kuhusu madhara ya rushwa, haki na wajibu wao, umuhimu wa kulipa kodi na kuepuka vitendo vya rushwa, umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo, wajibu wao wa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa pamoja na kampeni ya vunja ukimya kataa rushwa ya ngono hususani kwenye onesho la wafanyabiashara.

3.0 UCHUNGUZI NA MASHTAKA

3.1 UCHUNGUZI:

Kwa upande wa kazi za **Uchunguzi,** TAKUKURU Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba, 2022 imepokea **taarifa 126.** Kati ya taarifa hizo, **taarifa 106** zinahusu vitendo vya rushwa na **taarifa 20** hazihusu vitendo vya rushwa.

Kwa taarifa 106 zinazohusu rushwa taarifa 11 uchunguzi wake umekamilika na taarifa 95 uchunguzi wake unaendelea na uko kwenye hatua mbalimbali za uchunguzi.

Aidha kwa taarifa 20 zisizohusu rushwa taarifa 01 imehamishiwa katika idara nyingine na taarifa 19 wahusika wameelimishwa na kushauriwa.

Mchanganuo wa Taarifa zilizopokelewa kisekta

Na	IDARA/SEKTA	IDADI
1	Serikali za Mitaa	32
2	Utawala	21
3	Afya	11
4	Ardhi	9
5	Fedha na Mawasiliano kila moja sita	12
6	Idara ya Elimu na Siasa kila moja tano	10
7	Polisi	2
8	Mahakama na Maji kila moja tatu	6
9	Ujenzi, Hifadhi ya jamii, Ulinzi kila moja mbili	6
10	Biashara, Kilimo, Uvuvi,TANESCO, Madini, Ushirika	9

	Manunuzi, Magereza naTaasisi za dini kila moja, moja	
11	Taasisi binafsi	8
JUMLA		**126**

3.2 MASHTAKA:

Mchanganuo wa hatua mbali mbali za majalada ya uchunguzi

Na	HATUA YA MAJALADA	IDADI
1	Majalada yaliyopelekwa kwa DPP	05
2	Majalada yaliyopata kibali	05
3	Mashauri mapya yaliyofunguliwa Mahakamani	09
4	Mashauri yanayoendelea Mahakamani	27
5	Mashauri yaliyoamuliwa Mahakamani	11 na Jamhuri kushinda mashauri 09

4.0 MIKAKATI YA ROBO YA PILI YA 2022/2023

Mikakati iliyopo kwa kipindi cha Oktoba - Desemba, 2022 TAKUKURU itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria kama ifuatavyo;

4.1 Kuzuia vitendo vya rushwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ukaguzi na kusimamia kwa karibu matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi hiyo ya maendeleo.

4.2 Kuchunguza makosa ya rushwa kwa wale wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

4.3 Elimu ya mapambano dhidi ya rushwa, itatolewa zaidi kwa kwa njia ya vyombo vya habari (vipindi vya redio) na kwa utaratibu wa TAKUKURU MOBILE, yaani TAKUKURU inayotembea ili kuhakikisha kuwa TAKUKURU inawafikia wananchi moja kwa moja katika maeneo yao na kuwaelimisha juu ya umuhimu na wajibu wao katika kusimamia miradi ya maendeleo kwani tunaamini njia hii ni muhimu na itaongeza wigo wa ushirikishwaji wa wananchi kwenye Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

6. HITIMISHO

Tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mwanza kwa ushirikiano wanaotupatia na kuifanya kazi ya Mapambano dhidi ya rushwa kuwa na mafanikio. Tunazidi kuwaasa kujiepusha na vitendo vya rushwa na kuwa tayari kuwafichua wale wote wanaotumia nafasi zao kujinufaisha kwa njia za rushwa ili hatua ziweze kuchukuliwa. Kila mwananchi anapaswa kuibeba kwa vitendo kauli mbiu yetu ya mapambano dhidi ya rushwa isemayo :-

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU: TUTIMIZE WAJIBU WETU.

"Kwa taarifa za vitendo vya rushwa tafadhali fika Ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe au piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga *113# fuata maelekezo" Huduma hii ni ya BURE.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU.

IMETOLEWA NA:

JAMES RUGE
MKUU WA TAKUKURU (M)
MWANZA
0738 150 162